APAO VILLAGE MOPE

Sustainable Green Cover (KGC) Program

# SERA INITIATIVE

Sustainable Environmental Reforestation and Adaptation (SERA) | The Carbon Offset Projects






JOIN AND SUPPORT THE MOVEMENT

JOIN THE GROUP +255713764522

Panda Mlonge mmoja kwa wiki hapo nyumbani kwako, kando ya njia au barabara karibu na nyumbani kwako

# TUIRUDISHIE MITI ILIYOKATWA

APAO na MOPE kwa kushirikiana na familia na serikali za mitaa tumejitolea kuamasisha, kueleimisha, na kupanda miche ya Mlonge kupitia familia yaani "Agroforestry" na tunalenga kupanda miche zaidi ya 1,000,000 kila mwaka. Tumechagua Mlonge kwa sababu hauaribu shamba na una manufaa mengi kama kuuza mbegu na majani, kulisha mifugo, kupata dawa, kulinda mipaka ya shamba, kupata kivuli, kujali malazi ya ndege, na nyuki kupata maua ya kutengeneza asali.
Sisi tumeshapanda Milonge zaidi ya 500 kuizunguka APAO Village na tunaendelea kupanda. Tunatafuta familia zaidi ya 30,000 Kigamboni kuungana nasi kila wiki ili zituunge mkono kwa kupanda mlonge mmoja kila wiki kila familia kuzunguka shamba lao, kiwanja, kando ya njia au barabara karibu na nyumbani.

## 1. Miti mingi imekatwa, na inaendelea kukatwa pote nchini.

Miembe, miarobaini, mikorosho na miti mingi ya asili pote nchini imekatwa ili tupate mbao, kuni, na mkaa. Hii ndo njia nyepesi ya kujipatia kipato na nishati ya kupikia, lakini sasa miti inazidi kuisha, viwanda vinaongezeka na mabadiliko ya tabia ya nchi yako mlangoni kwetu.

Haya yote yanapelekea ukame, ukosefu wa chakula na maji, mmomonyoko wa udongo na hewa ukaa. Matokeo yake jamii kupatwa na njaa, umaskini wa kipato, magonjwa na kukosa hewa safi na hivyo maisha yetu kuwa ya wasiwasi sana yanayokabiliwa na matatizo yanayotokea kwa sababu ya mabadiliko ya tabia ya nchi, kisa kukatwa miti hovyo.

## 2. Lakini tunalo la kufanya kuinusuru hii Dunia, ni kupanda miti.

Kwa pamoja tuungane kupanda miti ili tuirudishie miti yote iliyowahi kukatwa miaka ya nyuma. Tunafanya hivyo kwa kupanda MLONGE, mti huu ni wa ajabu sana ambao hautoi mbao, mkaa wala kuni, hivyo mti huu utadumu. Na ni mti amboao unavumilia sana ukame na unaota vizuri sana popote nchini Tanzania.

Mlonge ni mti wa ajabu na hata umepewa majina yenye sifa kubwa kama "Tree of life na Magic tree". Hii ni kwa sababu mti huu unaweza kusafisha hewa ya ukaa kuliko miti mingine, uzuia mmomonyoko, unaleta mvua, unazuia upepo, na unaweza kupandwa pamoja na mimea mingine shambani bila kuathili mazao.

**AMKA** tuokoe Dunia yetu kwa kupanda Mlonge nyumbani kwako au kandokando ya barabara karibu yako, ukipanda mti wa mlonge piga picha na tuma kwa WhatsApp kupitia group letu la namba hii, +255713764522. na chini ya picha andika maneno haya hapa chini:

#amkaokoadunia #carbonoffset project